

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

TIGANIA WEST CONSTITUENCY, HELD AT KIANJAI POLYTECHNIC

ON

15TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, TIGANIA WEST CONSTITUENCY, HELD AT KIANJAI
POLYTECHNIC ON 15TH OCTOBER 2002.**

Present:

Com. Domiziano Ratanya

Secretariat Staff in Attendance:

Solomon Anampiu - Programme officer
Mary Babu - Verbatim Recorder
George Kimathi - District Coordinator

The meeting started at 10.55 a.m. with Commissioner Ratanya in the Chair.

Mr. George Kimathi: Habari ya asubuhi? Ninafikiri tutaanza mkutano wetu. Lakini kabla hiyo nitamuomba Bishop Mbogori atuongoze kwa maombi.

Bishop Mbogori: Na tuombe. Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, kwanza tunakushukuru na kukutukuza kwa vile wewe ni Mungu wetu, kwa vile unatupenda, na unapenda nchi yetu. Ni wewe ulituumba, na ulituumba ukatupa akili ya kuweza kuendelea kwa mapatano, kupendana, na kuishi pamoja. Tunajiweka mikononi mwako wakati huu ambapo tunafikiria mambo ya Katiba ya nchi yetu, Katiba ambayo tunataka ituelekeze katika mwenendo mpya, mwenendo wa amani, mwenendo wa maendeleo, na mwenendo wa kufikiria masilahi wa kila mmoja wa nchi hii. Tunakuomba kwanza utupe amani, utupe ufahamu, na utupe upendo katikati yetu, tukijadiliana mambo yote tuwe tunasikilizana, na tunaweza kupatana kwa yale ambayo tunaona unatupasa tuyafanye.

Ikiwa kuna jambo lolote lina hitilafu iwayo yoyote, utuongoze katika hekima yako, ili tuweze kuiona na kueleza kwa amani. Tupe upendo na wale wanaotuelimisha uwape ujuzi ili watuongoze kwa amani. Na katika kila jambo tunaomba amani yako hapa kwetu na katika nchi ya Kenya yote. Kwani tunaomba na kuamini katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu – Amen.

Mr. Kimathi: Asante sana Bishop. Kuanzia nitasema ya kwamba nafikiri nyote mwajua kwa nini temekutana hapa leo. Kuna Commissioner kutoka headquarters, na ako na staff wengine kutoka headquarters, na wamekuja hapa leo kwa sababu ya kutueleza zaidi juu ya Draft Constitution, ama Kielelezo cha Katiba ambacho mko nacho, in the Draft. Sababu ni kwamba wangetaka tuiangalie pamoja ili watupe muelekeo, ambayo utatuwezesha kusoma hii Draft Constitution, na kama kuna swali, twatarajia Commissioner yuko hapo, na sote tuko hapa na ma staff wengine. Tutaweza kujadiliana sote, na tupate huo muelekeo kujua zaidi.

Kisha kama kuna mtu ambaye atakuwa na la kuongeza ama la kutoa katika hii Draft Constitution, kama mjuavyo ni kwamba tutakuwa na delegates meeting, mwisho mwezi huu, mnaulizwa kama kuna jambo la kuongeza ama kutoa, muandike maoni

hayo ili yawasilishwe kwa Constitution Review Commission. Hawa Commissioners wataangalia mapendekezo hayo pamoja na delegates ambao watakuwa kwa Conference, ili yawe katika ile final document ya mwisho ambayo ni katiba mpya.

Kabla sijamualika Commissioner, ningetaka kuwajulisha wanakamati ambao tumekuwa nao hapa Tigania West. Tuko na na Jerusha Muyudhi, hawa ni 3 Cs members, ama ni Constituency Constitution Committee members. Then tuko na Mary Nairumbi, kuna Councillor Geoffrey Githai, halafu tuko na Geoffrey Toroitich, na pia tuko na huyu Madam anaitwa Beatrice Biariu, anatoka Igembe Constituency, ambaye hata ni delegate, ambaye ataenda huko Nairobi kujadili juu ya hii ya Draft Constitution. Halafu kuna mwingine, Kiambi. Hawa ni wale ambayo tumekuwa tukisaidiana nao katika kufunza mambo ya katiba hapa Tigania West, na kuna hata wengine lakini hawaja fika. Pia kuna Civic education providers, kuna wengine ninaona tuko nao hapa, lakini tuko wengi, na wakija nitawajulisha wote.

Langu ni kwamba ninataka tu kuwaomba, msikilize kwa makini yale Commissioner atatueleza, na wenzake, ili tutakaposoma hii Draft Constitution, tuelewe vizuri, kwa sababu kama mjuavyo, katika sheria, huwezi kusoma hapa three quarter ya hii document na uanze kuikashfu ama kutoa maoni yako. Lazima usome kila kitu ambacho kiko katika sheria. Kwa sababu unaposoma kitu fulani, cha kwanza, halafu hicho kifungu kiwe na mabadiliko katika kifungu cha huko mwisho. Utaona kuna wengine wanasoma halafu mara moja anasoma pages tatu, anaanza kutatisha hata bila kusoma. Kwa hivyo ningetaka msikize kwa makini ili mjue kama wale mnaojua wanashtumu bila kusoma. Pia niko na office assistant wangu anaitwa Banake Francis, yeye ndiye ananisaidia katika ofisi yangu huko. Wale ambao hawanijui ninaitwa George Kimathi. Kwa hayo machache nitamualika Commissioner ambaye atawajulisha wengine, na kisha atupe muelekeo, ama yale ambayo anapasa kuzungmuzia leo.

Karibu Commissioner.

Com: Ratanya: Asante sana Bwana Coordinator. Kama vile Bwana Coordinator, ameanza ninaona kwamba tumeanza kukubaliana hata lugha ambayo tutatumia. Kwa hivyo hicho ndicho kitu cha kwanza, tutakubaliana tutatumia lugha gani, kama ni Kimeru, kama ni Kiswahili, kama ni Kiingereza. Ukiangalia pengine kuna wale pengine hawataelewa sana Kiingereza, tukiendelea kwa Kiingereza kwa kila kitu. Tukiongea kwa Kimeru kwa kila kitu, tuna report hapa ambayo nitawajulisheni baadaye majina yao, ambaye hajui Kimeru, lakini Kiswahili atasikia, hata Kiingereza. Kwa hivyo pahali tumekuwa tumekubaliana tutumie Kiswahili, ama Kiingereza, na kama huwezi kabisa, unaweza kuongea Kimeru, tutatafsiri, kwa sababu maana ya mkutano huu, si kuja pengine tusome Kiingereza, Kiswahili, na wengine waende bila kujua tunasema namna gani. Maana ya mkutano huu ni kila mtu ajue tuko hapa na tunataka nini na tunafanya nini. Kwa hivyo tumekubali lugha gani? Kiswali. Ukiwa una kitu ambacho unataka kufafanua kwa Kiingereza uende kwa Kiingereza, si namna hiyo? Lakini kitu cha maana ni kwamba tujaribu kusikizana.

Baada ya hapo nitaendelea sasa na introduction yenyewe. Wale ambayo tumetoka nao Nairobi, kuna programme officer upande huu wangu anaitwa Solomon Anampiu, hata yeye ni wa kutoka upande wa Meru, upande huu wetu na ni Kibirichia. Bwana Solomon baadaye pengine atawasalimia wakati wake ukifika nitampatia nafasi. Kwa hivyo ni Programme Officer wetu

ambaye yuko huko headquarters katika Secretariat na tunaandamana na yeye..

Solomon Anampiu (*in Kimeru*)

Chorus:

Com. Ratanya: Na mwingine ambaye tunaye ni Mary Babu ambaye ni recorder wa haya tunaongea hapa. Kuna kitu ambacho tuna-record nacho, kuna machine hapa, ile ingine imeharibika, yaani stima pengine haikutaka kuingia vizuri, kwa hivyo tukasema tuendeleo tu kwa sababu kuna recorder ingine. Anaitwa Mary Babu, na ni officer wetu wa headquarters.

Mary Babu: Habari zenu wananchi?

Chorus:

Com. Ratanya: Na mimi mnanijua nimekuja hapa wakati tumekuwa na kazi ya process, na tena mimi ni mtu wa hapa. Mimi ninaitwa Domiziano N'Chokera Ratanya. Ukitaka kuniita, niite Chokera, hata Chokera iko, ingine ni Ratanya Domiziano, yale unataka kuniita. So I am the Commissioner.

Kwa hivyo tutaanza sasa mkutano wetu na kutoka sasa ningetaka kutangaza rasmi hiki kimekuwa kikao cha mkutano wa Constitution of Kenya Reviews Commission. Na mjue kwamba tukianza kikao chetu uko free kuongea chochote bila kuogopa, bila kufikiria utashtakiwa, kwa sababu tunasimamiwa na sheria. Kwa hivyo hiki ni kikao chetu cha Katiba na hakuna cha kuogopa, na tumeanza sasa, na ikifika wakati wake tutafunga kama vile ilivyo kawaida.

Katika mkutano huu hatutakaa sana na nitawaeleza maana ya kuja siku ya leo. Na hapa sasa nitaketi tuendeleo sasa na mazungumzo. Kwanza, ningetaka mjue kwa nini Commission imekuja hapa siku ya leo. Tumekuwa tukija kila wakati tukiwa na sababu. Today kama ningesema kidogo kwa Kiingereza, the objectives of the visit is to launch the National Report and Draft Bill of the Constitution of Kenya Review Commission and also to facilitate the public debate. Mtaendelea kutoka leo, nikiwaelzea yale ambayo tunayo, kusoma hiyo Draft, na muendeleo kuzungumza nyinyi wenyewe, in groups, individuals, na baadaye, wewe mwenyewe utaandika report ukitaka kuuliza maswali yoyote. If you have anything you would like to amend in this Draft, you make your own comments, and you send through the Coordinator, and then everything will reach us in Nairobi, and it will go to the National Conference. Kwa hivyo mmesikia sababu yetu ni kuja kumuonyesha kwamba tumetoka na Draft, na Draft ya Constitution, na hiyo si kusema ya kwamba ni final, si mwisho. Kwa sababu watu wangeuliza, sasa Constitution imetoka? Constitution haijatoka, tuko katika mpango wa Constitution itoke yenyewe hivi karibuni. Ile tumetowa ni hii tunaita Draft Bill ya Constitution, ambayo tunapendekeza, Constitution mpya. Hii iko katika hii karatasi ni Draft Bill ambayo ni utaratibu moja ambayo tutafuata, tukimaliza hapa tutaenda pahali ingine. Tukimaliza hapo pengine tutakuwa na katiba yetu

mpya. Kwa hivyo msije mkasema kwamba watu waende kusema kwamba tumewaletea Katiba hapa Tigania West. Lakina nimewaletea Draft yaani maandishi pale tumefika ambayo yakiendelea kutengenezwa, yatatoka na Katiba yetu.

Na kutoka siku ya leo, ama niseme kutoka siku ambayo tuli-launch tuliwapatia wananchi wa Kenya kutoka Commission. Tuliwapatia wananchi wa Kenya report ya kazi yetu tarehe ishirini na saba mwezi wa sita. You can read on this Draft Constitution, on top page ya kwanza. *Dated and issued at Nairobi at 11.00 am on Friday the 27th day of September 2002.*

Siku hiyo ndiyo tuliwapatia wananchi wa Kenya wote, 30 million, kujua kwamba kazi yetu pale tumefikisha. Yaani tumetoka na report yetu. Ile kazi tumekuwa tunafanya, tuliwajulisha wananchi wa Kenya kwa sababu Commission yetu, ile sheria ambayo ilituchagua, Act of Parliament, Cap. 3 (a) laws of Kenya, sheria hii, ilituambia sisi tuta-report kwa watu wa Kenya. Haikusema tumpelekee mtu fulani ili aangalie na yeye aende afiche halafu aseme imepotea. Hii imetuambia tukimaliza, tukifanya yale mapendekezo ya Katiba, tuwaambie watu wa Kenya. Kwa hivyo tarehe 27 ndiyo tuliwaambia watu wa Kenya kwamba tumeandika Katiba, tumefanya mapendekezo.

Kutoka siku ya leo kulingana na hii Act ambayo inatutawala in this Commission, tutaendelea na mazungumuzo kwa siku 30, thirty days, na hiyo ni kulingana na sheria. Tunasema, vile ambayo imebadilishwa, kwa sababu ilikuwa 60 days, lakini ikawa na amendments kidogo, ambapo kwa hiyo amendments, inasema kwamba tukitoa Constitution Draft, watu wataendelea kuzungumuza kwa siku 30. Lakini kwa ile ya kwanza ilikuwa 60 days. Lakini kwa sababu hata hiyo ni amendment ya Parliament, ni sheria. Sasa sheira inasema tukitoa hii tupatie watu wa Kenya waendeleo kusoma, kujadiliana kwa vikundi wao wenyewe individuals, kwa organizations zao, kwa siku kama 30 days. Na ukihesabu kutoka 27th September, siku thirty ama thelathini itaisha siku gani, kutoka 27th September? Si itaenda kuisha mwezi wa kumi, that will be on 27th October. Sasa 27th October, kutoka hapo sasa sheria hii ambayo inatutawala inatuambila vile tufanye kazi, inatuambia kuwe na mkutano wa Kenya yote. Wajumbe wa Kenya wote, si wajumbe, ni wale delegates watachaguliwa kwakilisha na kufanya huo mkutano wa katiba, unaitwa Constitution National Conference ambao utakuwa tarehe ishirini na nane mwezi wa kumi. So you see you have 30 days from 27th September, the day we launched this one to all Kenyans. Tuli tangaza ikaenda kwa magazetti, siku hiyo ikaenda kwa maradio, ikaenda kwa ma TV, na ikaenda kwa kila mtu.

Sasa tukiwa kwa Commission sisi wenyewe tukasema kwamba hata ingawa tumetangaza kwa Wa-kenya wote, na mambo yameingia kwa TV, yameingia kwa radio, yameingia magazeti, lazima tuje kwa wale ambayo walitupatia hii report. Wale ambao walitusaidia kupata maoni yao tukafanya hii kazi. Na hawa watu ni kutoka kwa constituencies. Tukasema haitoshi kutangaza huko Nairobi. Commission yenyewe ikaamua tuende round kwa kila constituency in Kenya, 210 of them. Tuna Constituencies 210, katika Kenya. Wale ambapo kuna MPs. Na moja yao ni hii Tigania West.

Sasa siku ya leo, kila area iko na Commissioner. Tumegawana sasa Commissioner mmoja mmoja a-cover karibu district mbili. Kama mimi nina-cover North Meru, and Meru Central. Na nili gusia Chuka, nilienda hata Chuka, kwa sababu ni Constituency moja katika Chuka. Kwa hivyo ninaweza kusema nime-cover three districts. Meru North, Central and Meru South. Kuna

wengine Commissioner mwingine pengine ana-cover district moja ambayo ina constituencies nyingi zaidi. Kwa hivyo tuko mmoja mmoja na maana yake ni kuwaletea hii draft.

Nyinyi tunawaambia kutoka leo sasa ambayo tumefika hapa Tigania West, tumefika kwenu kuwaambia ile report ambayo tulitangaza 27th, imefika hapa, na endeleeni na nyinyi kujitayarisha kusoma hii. Mfanye mapendekezo, na ikifika 30 days, tarehe ishirini na nane ambapo Conference itanza Nairobi mtakuwa mmepeleka maoni yenu yale mnataka huko Nairobi. Na njia ya kupeleka ni kwa Coordinator, na Coordinator atapeleka huko kwa Secretary, akina Anampiu na Secretariat itapanga, ilettee Commission, nayo itawapatia delegates ambao watakutana tarehe 28. Kwa hivyo hiyo ndiyo maana sasa ya mkutano kama wa siku waya leo. Nitaendelea sasa kupumzia hapo; na siku ya leo hatuna mambo mengi, tumepewa hata masaa mawili tu kuwa na nyinyi ili muende mkasome na mkafanye mipango yenu ya kufanya debate. So for us we have to launch and facilitate the debate for these 30 days ambazo tutaendelea.

Kitu ningetaka kuwakumbusha hapa hata kwa Draft, ingetoka hata kwa Kiswahili, lakini version ya Kiswahili inaendelea kutengezwa, pengine iko tayari sasa lakini mtapewa baadaye. Tukasema tuanze na hii ya English na ya Kiswahili itakuja baadaye.

The other thing, pengine mtauliza, kwa nini haikuwa katika kitabu, kama hiki, ama kitabu kingine kama vile kitabu cha sheria kinawekwa namna hii? Tuliona kwamba, hatuwezi kuenda kuweka kitabu ni very expensive kwanza, kwa sababu maoni yale yako hapa yanaweza kugeuka. Mukisoma muone kuna kitu tumeacha, you can amend, yaani mnaweza kubadilisha, mnaweza hata kutuma maoini tofauti. Yale ambayo tumesema hapa, pengine mngesema haya maoni hayatoshi, mngeongeza ama kuondoa. Sasa tukasema tutoe kwa njia hii ambayo ni cheap, ambayo ni rahisi. Tukakubaliana na newspaper Nation, na ika-print hii kitu ambayo tutapeana kwa kila Constituency. Kila Constituency tunapeana kama 60 to 70 copies na copies zingine zitakuja kwa documentation Centre. Pengine wakati huo kabla tumalize mwezi moja, mnaweza kuwa na bahati, kuwe hata Swahili kitakuweko. Kama yeyote akiona hapati copies, kwa sababu ilikuwa kama 70 hivi na ndiyo tunapeana kila pahali, tutakuwa na zingine zitakuja. Bwana Kimathi, I think unaweza pengine kuangalia, kwa sababu tumekubali zitakuwa kwa Documentation Centres. Na mtachukua. Sasa wale wanazo wataendelea kusoma.

Now kabla ya kuja kwa hii Draft, kwa sababu sasa hii ni draft ya Constitution, mapendekezo yale yamewekwa. Tulipokuwa Mombasa tulitoa report ya kwanza. Na hiyo ndiyo tulikuwa tunaita short report. Report fupi, ilikuwa inaonyesha, ama inakumbusha wananchi pale tulipoanza na vile tulipoendelea. Na hiyo report, hata hiyo ilitokea kwa gazeti kama hii, pengine watu walinunua. Kwa sababu tulitoa hii tarehe 18 mwezi wa tisa, tulipokuwa Mombasa. Hiyo iliwezekana tukaweka kitabu kama hiki, ambayo tunaita short version ya report, the Report of the Constitution of Kenya Review Commission. Hii ndiyo ilitoka kwanza, kabla ya Draft yenyewe, kabla ya Katiba yenyewe. Hii si ndiyo Katiba, lakini ni report ya kupeana tu highlights vile tulipoanza, ni kukumbusha watu vile tulianza. Ni report tu ya kuonyesha kwamba tulichagua Commissioners hata majina yako hapa, tukaendelea tukafanya Civic Education. Na hizi copies ziko kwa documentation centres, ni chache ambazo ziko

huko. Tukaona na kuangalia kidogo mambo ambayo watu walikuwa wanakubaliana katika Kenya yote, in short it is a sort of short report. Kwa mfano kama ni kutoa hapa 13 main points from the people, yaani points ambazo watu wote katika Kenya. Not only 13-lakini ni nyingi, walikubaliana karibu wote. Point kama hii, kwa mfano, “We do not want power concentrated in the hands of one person. Hatutaki mamlaka ama na nguvu yote ikae kwa mtu mmoja.” Katika Kenya yote, hata hapa na kila pahali walisema hivyo. Wakasema kama kuna ukubwa, kama kuna utawala, ama power nguvu yoyote ya kutawala watu wa Kenya isiwe katika mkono wa mtu mmoja. Awe yeye ndiye ni pekee anasema. Lazima hiyo nguvu igawanywe watu washirikiane kila mtu awe na kitu cha kufanya ili kuweza kutawala Kenya. Point kama hiyo ilikubaliana kila pahali. Tukirudi kwa hii report yenu yenyewe mtaona pengine kuna point kama hiyo ilitoka hata hapa.

Watu wa Kenya walisema, we want an end to corruption. Ufisadi, hii ni birbery, hii kitu inaitwa kidogo kidogo hii. Watu wa Kenya wanasema hatutaki hiyo. Na kitu kingine kama, we want women to have equal rights and gender equity. Hata akina mama wanaona kama wako chini wakati mwingine mambo yao hayaangaliwi vizuri, lakini watu wa Kenya wanasema, tunataka waonekane kama binadamu na wao wafanyiwe kama watu wengine. We want respect and decent treatment for the disabled. Watu wengine ambao wanafinywafinywa ni disabled ambao ni watu hawajiwezi kama wale watu ambao hawana macho, watu hawana miguu, unajua wale watu wasiojiweza. Hata hawa inasemekana, wawe wanaheshimiwa, na hawa yako kwa katiba. Kwa sababu ninawaambia si Katiba. Kwa sababu hii ninawaambia hii Katiba, ni just short report ya kuonyesha kitu ambacho generally kiko kwa katiba ndani. Na kama hii tunasema we want respect and decent treatment for the disabled. Katiba itaonyesha ni namna gani hawa watu wapewe heshima. Kama ni sheria itafanya ili wapewe heshima iko hapa. Kama ni kuonyesha taratibu itafuatwa wapewe heshima inonekana hapa. The same case with corruption. Kwa sababu watu wa Kenya wanasema hawataki corruption. Sasa Katiba yenyewe, Draft yenyewe inaonyesha ni njia gani tutatumia ili corruption iishe. Kama ni sheria itatengenezwa, kama ni Commission, kama ni nini, hayo yote yako hapo. Kitu kingine kama very general ni kitu kama, “We want our MPs to work hard, to respect us and our views and the power to kick them out they do not perform.” Hata hiyo point ilitokea kila pahali.

Watu wanasema tunataka ma-MPs wetu watuheshimu. They are our representatives. Yaani ndio tunatuma kule, hatuwezi kwenda huko Nairobi Parliament sote. Mtu mmoja anatumwa kwa constituency ili angalie mambo yetu. Tunataka atupatie heshima. Na tukiona huyo mtu hawezi kuendelea, hatuwezi kukaa miaka tano tukiwa na mtu kama huyo. Kwa hivyo hii katiba imetoa njia ya kuondoa mtu kama huyo. Hata akiwa amekaa mwaka mmoja muone hamuwezi kuendelea, hii Katiba ya sasa imeonyesha ile njia mtafanya. You remove him, you recall him, na akija mtatafuta mwingine. Point ingine ambayo ni very general, “We want a fair system of access to land for the future and justice for the wrongs of the past. Yaani kwa mashamba tunataka mambo yafanywe kwa njia nzuri, kama ni kupata mashamba, na kama ni kufanya ma-case, kama ni tuone njia ambayo watu watapata mashamba, na mambo ambayo yamepita yarekebishwe. Na hayo yote kuhusu mashamba kama hiyo yako hapa. Na mtaona mkifika hapa kuna ile tunaita Land Commission of Kenya ambayo haikuwako lakini itakuwako sasa, na ndiyo ita-address haya mambo yote.

Kitu kingine general kabisa ambacho tulisikia kila pahali, we want all communities to be respected and free to observe their cultures and beliefs. Watu, tamaduni zao zile zinalingana na Katiba na sheria hatuwezi kuwaambia waache ama kuwalazimisha. Lakini kama kuna utamaduni zozote ambazo zinakataa the Supreme Law, hii sheria kubwa ya katiba, hiyo tamaduni haiwezi kuwako. Na mnajua hata sheria yenyewe kama kuna sheria inafanywa ambayo haikubaliani na Katiba hiyo si sheria. Kwa hivyo kama kuna tamaduni zitapatikana pahali, ama sheria pahali ambazo hazishirikiani na Katiba, hiyo haiwezi kukubaliwa. Lakini ambazo hazina mambo na Katiba, hazina ubaya, hiyo ni sawa sawa tu hakuna taabu. Na ile mbaya lazima iondoke, na hiyo inaonekana na wananchi, wanaona ni sawa sawa, itaendelea. Kwa hivyo hatuwezi kusema kama ni cultures ama hii itoke en-mass, ati wewe uwe Mustralia ama uwe Muamerika, hapana. Wewe ni mtu mweusi, hata rangi yenyewe ni mweusi. Na hiyo lugha yako ni lugha yako. Vitu kama hivyo huwezi kujiondoa kutoka kwa wewe. Hamjui kwamba hata lugha ni cultutre. Hata utaona baadaye utaona lugha yetu ya Kiswahili imepewa mamlaka zaidi zaidi ya yale ilikuwa party ya utamaduni yetu. Yaani lugha yetu.

So kwa hii report hiyo ni point na moja ninawaambia sisomi yote ni just to highlight. Kuna pahali pengine, kuna maoni. How is the new Constitution different from the old? Ile kazi ambayo sisi tumefanya is the Review of the Old Constitution, what we call the current Constitution. Kazi yetu ilikuwa ni Review ya hii, na si Commission walifanya Review pekee yao. Waliambiwa maneno ambayo watafanya Review kutokana na nyinyi kutoka every constituency. Na kwa hivyo, ukiangalia just at a glance utaona mambo kidogo kidogo ambayo mkiangalia hii Draft, mtaona yanakuwa tofauti na hii Katiba ambayo tunayo sasa. Kwa hivyo hii ikitoka utaona there will be some differences. Tutakuwa na mambo mengi yatageuka. Na yale tunaona ni sawa sawa kwa ile katiba ya zamani, yatakuwako. Lakini yale ambayo wananchi wametuambia tupindue, tubadilishe, yamebadilishwa. Na hata ningetaka kuwaambia mfano mmoja, si mmoja, ni kama miwili; mitatu.

Parliament will consist of two Houses: the National Assembly, and the National Council. Hiyo ndiyo tofauti moja kwa hii sheria, hii Katiba hii, this is the current Constitution. Parliament ni moja, just one National Assembly, with 210 constituencies, na 12 ambayo wamechaguliwa, nominated. Lakini kwa hii Draft yetu ikitoka na ikuwe katiba, tutakuwa na 2 Houses katika Parliament, Parliament itakuwa nyumba mbili. Tutakuwa na National Assembly, ile tumeandika iwe jina lake ni National Assembly, na ingine tumependekeza iwe ni National Council. Zamani kulikuwa na, wale wanakumbuka Lancaster House Constitution, kwa sababu hii ambayo ni current tunayo ilitokana na Lancaster House Constitution, ambayo imefanyiwa a lot of amendments mpaka imekuwa vile ilivyo. Lakini ilitokanana Lancaster House, 1962-3 there. Wakati huo tulikuwa na Upper House ambayo ilikuwa inaitwa Senate, na kulikuwa na National Assembly or House of Representatives ambayo ilikuwa inaitwa pia Lower House, tulikuwa na mbili wakati huo. Lakini kutoka uhuru, wale ambayo walichukua ukubwa ama uongonzi wakasema hebu tubadilishe hii maneno ya kuwa na nyumba mbili, yanaharibu nguvu yetu. Wakaweka amendment, amendment ya kwanza ilianza kupindua kutoka Prime Minister, na President. Kutoka na Governor General ambaye alikuwa Mzungu alipoenda tulipopata Republic, we started immediately with President without Prime Minister, sasa hiyo ilikuwa first amendment. Ikaendelea zingine.

By '66 around there, ikafanywa Lower House, ibaki peke yake, Upper House ikaondoka. Na area hii tulikuwa na mjumbe wa Upper House, isipokuwa hakuwa representative wa hapa, alikuwa upande wa Isiolo, Bwana Langwe, sijui kama amekuja hapa siku ya leo. He is an example. He was a Senator, alikuwa Upper House. Lakini walifanyiwa mabadiliko, ikawa amended wakaondoka. The House of Representatives. Walipoona ya kwamba hiyo amendment imefanywa, kwa sababu ilifanywa around 66-7, wakaona hawawezi kufanya election 1968. Na hapo ndiyo mara ya kwanza tunajua the only time period ya parliament ilikuwa extended, na sababu ilikuwa they wanted to know how they can accommodate the Senators, because they had already removed the Senators by an amendment. Wakatafutia Senators Constituencies, akina Lawi, akina Muthamia, hawa ndio ninakumbuka walikuwa upande wa Meru, kwa sababu muthamia alikuwa hata Meru, kwa sababu alikuwa mmoja alikuwa wa Meru District, alikuwa Senator wetu, Julius Muthamia. Lawi alikuwa Isiolo. Na kuna wengine wa Nyeri, akina Mathenge, sijui wa upande mwengine. Sasa kwa sababu waliambiwa waende nyumbani, then there was need to extend parliament, na instead ifanywe 68, ikafanywa 69. So mtaona huo ni mfano kwamba tutarudia hiyo sasa, two Houses in our current draft, there is that recommendation ya kuwa na nyumba mbili.

Tukienda kwa point ingine, a person does not have to be a member of a party in order to stand for election. Hata hiyo utaona iko kwa Draft yetu, hata ingawa wewe huendi kwa party yoyote kama KANU, kama hii inaitwa NAK ama what, tunasikia hata ingine ilitoka jana, inaitwa sijui Liberal Democratic, kitu kama hicho. Hata ingawa hauko kwa hizi parties zote, hii draft yetu proposal yetu mpya inasema unaweza kupigania kiti cha bunge ukiwa kama independent candidate. Na ukiona mambo kama hayo yalikuwa 1964, kama kuna yeyote pengine, sisi ni wazee wengi sana hapa wanakumbuka haya. Tulikuwa na independent candidate, mnakumbuka 1963 elections. Mzee Ithaigwa ndiye alikuwa independent candidate, mnakumbuka wale wazee walikuwa huko. Ithaiga alipuigania kama independent candidate, hakuwa KANU, hakuwa KADU, ama ile party ingine APC ya Ngei. Yeye alipigania kama independent candidate, lakini alishindwa na mjumbe wa party ya KANU ambaye alikuwa anaitwa Washiara. Abraham Washiara. Alishinda hata KADU, na akaenda Parliament. Sasa yatakuwa mambo kama hayo tu. Mtakuwa sponsored na parties lakini you can also be sponsored just by the people. Kutokana na watu waku-support, kama independent, uende upiganiae tu, na ukipata nafasi yako uwe kiongozi, uwe MP. So you can see that is a difference between new and old.

Ingingine ambayo mtaona iko kwa hii, mtaona kutakuwa na kitu kama, point kama hii, "the Administration Police are to lose their separate identity." Hata ingawa imekuwa worded namna hiyo si kusema Administration police wataondoka kazini, lakini wataingia kwa Police. Na kwa katiba hii, kuna Police wanaitwa Administration Police na Police wenyewe na wana sheria mbali mbali. General Police ama regular Police ni Cap 84 laws of Kenya na Administration Police ni 85 laws of Kenya. Kwa hivyo pengine itakuwa hivi hiyo Cap 85 itakuwa repealed iondoke kabisa, na Administration Police waingie kwa police. Wote ni Police, so it will be just a matter of deployment. Kwa hiyo mtaona ni tofauti, na itakuwa kwa hii Draft yetu mkiendelea kusoma ndani.

The president can be removed from office by a process of impeachment at the instance of parliament. Parliament inaweza sasa

kufanya impeachment, yaani njia ya kumuondoa President. Kama president akifanya makosa, tuna sasa katika Draft mpya njia ya kumuondoa, lakini kwa hii ya zamani, haikuwa na njia ya kumuondoa. Hata akifanya namna gani mnapiga makelele tu hivi. Mnanung'unika tu lakini anaendelea tu mpaka wakati wake unafika. Lakini kwa hii, kuna njia ya kumuondoa, hata akikaa mwaka mmoja miwili mitatu, pengine, kabla hata ya kumaliza kuina njia ya kumuondoa. Na hiyo ndiyo itakuwa sana mkiangalia kwa hii Draft, itakuwa sana kazi ya National Council.

The other point ni ya -- Provincial Administration will be abolished. Unajua ninaguza mambo moja moja ambayo hata ni ya mageni, ambayo watu wataona hata ni magumu. Lakini mliambia Commissioners wafanye Review kwa vile nyinyi wenyewe mlisema. Kwa hivyo Provincial Administration, yaani hii system commonly known as the Provincial Administration, ambayo inaanza kutoka Assistant Chiefs, Chiefs, D.O., D.C., P.C. na kwenda hata kuwa na Permanent Secretary ambaye anawasimamia, the whole of that system, hata sasa inaitwa office of the President. Hata mimi wakati moja nilipitia hapo. Kwa sababu ya waalimu, nilipitia hapo. Ninaona wengi hapa kama Bwana Zakayo Kamencho. Nilipokuwa ninaingia huko aliniambia niingie huko, kwa sababu alikuwa huko. You see. Sasa tulikuwa huko sote na wengine wengi. Sasa system hiyo office of the President, ile ambayo imetoka assistant Chief mpaka juu is commonly known as Provincial Administration. Na hayo ni mambo watu wanaona ni magumu sana. Na hii Draft inaonyesha vile wataondoka. Katika katiba inaonyesha, na imependekezwa iondolewe. Lakini si Commissioners walisema, ni nyinyi wananchi.

Nikitaka sasa kuona mambo kidogo pengine kutoka kwa yenu wenyewe; hii file iko maoni ya Tigania West. Tulikuja hapa tukachukua maoni yenu, kurekebisha katiba, review. Na maoni yenu tuliwaambia tutaleta, sasa yako hapa, although we have only one copy na yatakuwa kwa documentation center yetu. Pengine baadaye tatakuwa na copies nyingi kuonyesha yale watu wa Tigania West walisema. Nikiangalia kwa haraka sana, kitu kimoja nione kama ni Executive, watu wa Tigania hapa Kianjai hapa walisema the Constitution should limit the powers of the president. Nyinyi mlisema hivyo hapa. Hiyo ni kitu moja mlisema. Na katika Kenya tulisikia watu wengi wengi wakisema hivyo. Kwa hivyo tukilinganisha haya mambo yamesemwa na watu wengi, sasa yako hapa. Mpango umepangwa wa kupunguza hiyo power tena si nyinyi wenyewe mlisema? Sasa huo ni mfano mtaendelea kusoma kwa hii. Hata wakasema tena kwa hiyo hiyo. The Constitution should limit the duties of the President. Yaani wapunguze ile kazi zake. Hiyo ni the same, ni kama kusema powers, ile nguvu yake iendelee kupunguzwa.

Tena walisema hata ingawa sijui kama imekuwa namna hiyo lakini walisema, the Constitution should provide for a ceremonial president who shall not belong to any political party and should be elected by popular vote. Yale ambayo yenu ninafikiria yameingia kwa Katiba kutoka Kianjai hapa, kutoka Tigania West, mumesema he should not belong to political party. Hiyo imeingia kwa njia ingine. Kwa sababu president hata ingawa atakuwa kwa any political party fulani, hatakuwa anafanya hiyo kazi akiwa president. Kama akiwa ni Chairman, ataondoka hiyo, akiwa ni Secretary akiwa any official, he will leave all those things akiwa president, na atakuwa president wa watu wa Kenya. Na hapa mlipendekeza something similar to that. Na tena mkasema lazima achaguliwe na popular vote. That one is in the Draft, kwa sababu president atachaguliwa na hawa wote.

Lakini vile mlisema ceremonial president, we did not get a lot of support from all over Kenya. Kulionekana Kenya yote awe na power ya kutosha lakini si ile yote, iwe devolved, ingine iwe shared. Kwa hivyo president Kenya kulingana hata na Draft yetu hatakuwa Ceremonial. Atakuwa Executive president lakini mamlaka yake yatakatwa, na mtaona kwa Draft vile yamekatwa, na watu wametoshika hivyo. Mlisema awe ceremonial na wengine walisema, lakini haikuwa very popular point. Pia ceremonial ni kuwa hana chochote, lakini anakaa kama mzee hivi tuu, pengine kama nikuchukua president kama wa Israel, na hata India. Sijui kama mnamjua, mnamjua? Hamjui president wa India, kwa sababu yule anafanya yote ni nani? Prime Minister.

Mchukue kama U. K. kama Great Britain kama Queen mwenyewe hiyo ni tofauti, Monarchy, hiyo ni tofauti sana. Lakini yeye ni ceremonial, lakini ana nguvu zaidi kwa zababu huo ni mfano mwingine, ni monarchy. Lakini Prime Minister tena anachukua mambo ya serikali yote.

Then ingine hapa Kianjai mlisema the Constitution should provide for a code of conduct for the president and Prime Minister. Hiyo imeingia sawasawa. Impeachment imeingia, hata njia ya kuondoa Prime Minister mtasoma hapo, njia ya kuondoa president mtasoma. Nione Kianjai hapa walisema lingine. The Constitution should provide a minimum qualification for a university degree for a president. Hapa hapa Kianjai watu walisema kwamba president awe wa kiwango cha university degree masomo yake, at least first degree. Mlisema hapa na wengine wengi walisema in Kenya, and we have put this one here in the Draft. Kwa hivyo president wa Kenya hatakuwa anything below the university degree, katika masomo yake. Hiyo tumesema lazima awe na hiyo.

The Constitution should provide that the president shall not be a neglecting MP, ndiyo hiyo mlisema hapa Kianjai hapa Tigania West, na hiyo iko hapa. Kwa hivyo president hatakuwa MP, atakuwa president wa Kenya. Na ukiangalia hapa, hata Ministers hawatakuwa MPs. This is also here. Watatoa watu kutoka outside. Tena kitu kingine ni kwamba the Constituton to provide that the president shall be between forty years and 70 years, wengine walisema 30 years to 75, 35 to 70, ama 35 to 75, tukaenda namna hiyo mpaka tukaweka kwa hii Draft yetu, tukaweka hata vile mlisema, kiwango cha mwisho ni 70 years. Lakini tulikubaliana iwe 35 to 70, hapo tumeweka kwa hiyo. Pengine hapo watauliza kama kuna interest fulani, kama inaweza kwenda juu zaidi, lakini hiyo itakuwa mazungumzo pengine ya National Conference. Ama ukitaka kupeleka comment yako, ukisema ni heri president awe 85, ama 90, ukisoma hii, hayo utapendekeza, na pengine ukienda National Confence, wale wajumbe, wanaweza kukubaliana ama kukataa.

Hapo sasa nimelinganisha hii mambo ambayo mlisema lakini sikusema yote yako mengi, na tutaenda, tutalinganisha na report yetu kidogo, just a highlight.

Hebu sasa tumalize hapo tuende kwa Draft yenyewe. Na kabla kuingia ndani ya hii Draft, nilisema tukimaliza kuzungumza debate ya 30 days, tutaenda kwa National Conference, na hii National Conference ninataka kuwakumbusha inachaguliwa namna hii. Kukoo na watatu kwa kila District, watu watatu kutoka kwa kila District, na mmoja awe mama. Sasa hii Nyambene

District ama North Meru imechagua watatu hawa, they are three. Mmoja ametoka upande ya Mkinduri anaitwa Mr. Mukeba, huyo ni delegate, na ni nyinyi mlichagua, mkisaidiwa na councillors, kulikuwa na hiyo system. Sisi tulikuwa tunangoja report Nairobi, na tulipata report na majina ya hawa wote wale mlichagua. Na mkachagua mama kutoka upande wa Igemba Constituency, Beatrice Bairu, huyu ni Beatrice Bairu ni mmoja wa delegates, kwa wale watatu, kwa sababu lazima mmoja awe mama. Kuna mwingine, na ninasikia ni Councillor kutoka upande wa Ntonyiri. Sasa hawa ni watatu ambao wametoka katika Meru North District. Na kila district kuna watatu, everywhere. Tuna districts 70, ukipata watatu watatu, those are 210 delegates halafu wengine members ni MPs, ambao ni 210, unaona nambo imeenda juu 420 mpaka hapo. Kutakuwa na wengine kutoka NGOs, political parties watakuwa 41. Zile registered parties wakati huo, kwa hivyo kutakuwa na 41, kutoka 41 political parties. Na hao si Members of Parliament, kwa sababu hawawezi kuwa parliament, kwa sababu parliament wako huko. Kama ni DP, si MP, ni mwananchi, lakini si MP. Kuna wengine wanatoka kwa NGOs, kuna wengine wanatoka kwa kikundi cha akina mama, religious organizations, na Commissioners wenyewe watakuwa huko. Commissioners ni 27, na two ex-officio Commissioners, Attorney General and Secretary, we are all 29, tutakuwa huko.

Lakini sisi hatutavote, because we cannot vote for our own Draft. Tutaenda tu kusikiliza vile delegates watasema. Kazi yetu itakuwa tu logistics kuorganize mambo, pengine kupanga viti na makaratasi. Lakini wale wakubwa ambayo watafanya kazi ya kupiga hata kura ni hawa delegates. Delegates wote watakuwa karibu 600--- I do not know the exact figure, kwa kuwa kuna corrections zilifanywa hapa na hapa. Lakini ni over 620 and above. Hawa watakutana Nairobi on 28th, baada ya kumaliza siku 30 za debate ya hii draft, halafu apelekewe comments, recommendations, new ideas, ya kugeuza hii na halafu wazungumzie kwa sababu watakaa hapo, kwa mkutano for 30 days yale watatoa ndiyo sasa watakubaliana kufanya final Draft Bill kupeleka kwa parliament, na iende parliament, hiyo ndiyo itakuwa stage ingine. Parliament ikimaliza ikifanya enactment iwe law, president na iwe law, siku hiyo hiyo Commissioners sasa wataondoka. Yaani hiyo Constitution ikiwa law kama hii ya kisasa, siku hiyo ndiyo Commissioners wataondoka. Halafu Constitution mpya ipatiwe sasa serikali ya Kenya na iendelee na kutekeleza sasa. Hiyo ndiyo process kidogo ambayo imebaki. Ukiangalia hapo utaona sisi Commissioners tumemaliza kazi yetu, kwa kuweka mapendekezo yenu yote kulinganan na sheria. Tuliambiwa we shall collect and collate, tumefanya hivyo, tumekuja kwa nyinyi, kuwaambia iko hapa. Maswali mengine watu wanauliza wanasema, election itakuwa na new Constitution ama old Constitution? Hilo si swali ambalo unaweza kumuuliza Commissioner, hiyo hatujui. Kazi yetu nini? Ni hii tumefanya. Hata serikali ikisema elections ziwe kesho, huo ni mpango sasa wa watu wengine. Hatujui hiyo sasa. Kwa sababu sasa yetu imekwisha. Na tumefanya vizuri sijui kama kuna watu watasema ni vizuri, sijui kama kuna watu wanasema si vizuri, lakini watu wengi wanasema mumefanya vizuri ikaisha mapema. Kwa hivyo hata kama elections zitakuwa kesho ama whatever hiyo si kazi yetu. Kwa sababu kama ni ballot boxes ambazo tumesema kwa hii Draft ziwe transparent, hatujui pale zitatoka. Hatujui tena ni nani atafanya Ulaya ama wapi. Kufanya hiyo all transparent boxes kwa all polling stations, hiyo si kazi yetu, itafanywa na wengine. Kama ni mambo ya ballot papers, mambo ya ballot boxes hizo ambazo ni transparent, hiyo yote ni mipango ya watu wengine si ya Commission. Kwa hivyo maswali kama hayo pengine Commission haingeweza kujibu.

Kile tu ningetaka kuwaambia kila pahali tumeenda watu wanataka tufanye elections na new Constitution, hiyo nimesikia. Na

hata sisi Commission tumekubaliana na hiyo. Ikiwezekana ifanywe na new Constitution, lakini hatuna mandate, hatuna nguvu ya kufanya hivyo. Lakini tunakubaliana na hiyo hata sisi.

Na tukiingia hata kwa Draft yenyewe, nikimaliza hii kwa sababu kuna programme kidogo, tutakuwa na wakati wenu maybe almost an hour ya reactions, ya questions na kila kitu when I finish my presentation. Yeah kwa report, kwanza I was talking about the report, short report, na hii ambayo mlisema na the general points which maybe are appearing here, kwa hivyo ninaona inalingana Bwana Councillor. Hii is just an introduction, just to show what is appearing here, and we are going there now, just to highlight. Then after that you can ask questions, kwa sababu unaweza kuuliza swali ambalo liko hapa.

The next point I will do now is to go to this Draft. Ukifungua page 2, na yale nitafanya kwa hii ni kuonyesha layout ya hii Draft report, na mambo mengine ni wewe utasoma, kwa sababu hatujakuja hapa kusoma. Hatuna wakati wa kusoma yote, mtasoma for all these days from now. Na wengine wamekuwa hata na kuendelea pengine kusoma. On page 2, kuna hapa table of contents, vile hii draft yetu imepangwa kuna Chapter 1, Sovereignty of the people and the Supremacy of the Constitution, hiyo ndiyo ya kwanza. Utaendela, kuna Chapter 2, na tena ninataka kukujulisha kwamba hii section katika Katiba hii, ilikuwa inaitwa section, but in the new Constitution we would like to call them Articles. Kwa hivyo kuna Chapter one, kuna article 1, inasoma namna gani, Sovereignty of the People, halafu unaenda number 2, Supremacy of the Constitution, enforcement of the Constitution, defence of the Constitution, the laws of Kenya. Sasa ukienda kwa six under chapter 2, nayo ina maneno mengine.

Sasa hii ni arrangement ninataka kuwaonyesha kwanza. From Chapter 1 kwa hii Draft yetu inaenda through to Chapter 20, on page three. Na hapo ndipo mnaona tunafika all articles we have in this Draft, we have 299.

Hii ya mwisho hapa ni ya muhimu sana, kwa sababu inaonyesha yale mabadiliko yatafanyika yatafanywa namna gani, ni taratibu gani ambazo zitafuatwa. This is why we have chapter 20 on page three. Transitional and constitutional provisions, yaani ule utaratibu tutatumwiwa kwa mabadiliko. Zile points nilisema za Provincial Administration nimesema kwa hii Draft zitaondoka. Provincial Administration huwezi kuondoka siku moja uende umwambie Chief toa uniform nenda. Tutakuwa na taratibu, na hii ndiyo Chapter 20 inaonyesha sasa transition provisions ambazo zitakuwa hata kama ni Provincial Administration wataondoka namna gani. Kama ni wale wamekuwa na age ya kutosha, wawe retired. Pengine wengine wawe wana discipline matters waondoke. Pengine wapelekwe pahali pengine kazi, wengine waende nyumbani. Namna hiyo tu kuna njia itaelezwa hapa. Kama ni D.Os, D.Cs, those are very qualified people, lazima watakuwa ni viongozi wanaweza kupelekwa pahali, ama wengine waondoke. Kwa hivyo hii unaelezwa kwa Chapter 20. Na wakati utasoma kwa sababu utasoma wewe mwenyewe utaona vile imelezwa. Na ukisoma chapter kama hii ukiona kuna mambo ambayo yamebaki you make your comments. Unaweza kusema kitu fulani fulani hakikuwako. This is why we are giving you this one to do it, huo ni mfano mmoja.

Na kitu kingine angalia page two, we have got preamble, kuna hapo katika page two kuna box moja hapo imeandikwa na jina Preamble, mumeona hapo? Hii Preamble, ni utangulizi, kind of introduction. Katika hii katiba ya sasa haina hiyo. Ukianza kusoma katiba hii wale wamesoma hii katiba, the current Constitution you can see the way it starts. Section one, Kenya is a

sovereign republic, mambo yameishia hapo. One way the Republic of Kenya shall be a multiparty democratic state. Unajua hii ni amendment ilifanywa baada ya kuwa multi-party, kutoka 92/98. It is a very recent revision, hata hii amendment. Inaenda inasema, the public seal of Kenya shall be such devised as may be prescribed or under Act of Parliament. So hakuna introduction, inaendelea straight away kwa provisions of the Constitution, kwa section. Sasa hiyo ndiyo tofauti na hii kwa preamble. And tulisikia kwa kila pahali, hata nyinyi wenyewe I think, the Tigania West hapa walisema na mambo yako hapa. Sasa tulichukua haya maneno kutoka kwa kila pahali, and then we agreed we have a sort of preamble. Na ukiangalia katika hii preamble, mambo yenu pengine yamewekwa hapo, maoni yenu, yamekuwa captured hapa kutoka Tigania West na kila pahali.

Hii wakati tunaenda round ndiyo wakati mwingine tungetaka hata mtu mmoja atusomee, because you should also participate kabla kukuja kwa maswali. We the people of Kenya—Preamble, nani anaweza kuji-offer atusomee hapa? Yes, hebu Mukula unaweza kusoma, utusomee kidogo na mwingine ataendelea.

Mukula: We the people of Kenya aware of our ethnic cultural and religious diversities, and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation, committed to nurturing and protecting the well being of the individual, the family and the community within our nation.

Com. Ratanya: Hebu mwingine asome.

Joseph Mutuma: Recognizing the aspirations of our women and men for a government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law, exercising our sovereign and inalienable right to determine the form of governance of our country, and having fully participated in the Constitution making process, do adopt, enact and give to ourselves---

Com. Ratanya: Just stop there, and let somebody else read.

Mzee David Muirebwa: --- do adopt and enact and give to ourselves, and to our future generations the Constitution. God Bless Kenya.

Com. Ratanya: Mnaona hata Mzee baba anasoma kwa sababu alienda shule, aliingia kwa class- room. Sasa do you like that Preamble? Mnona ni sawasawa hiyo? Kama mtaona kuna kitu tunataka kuongeza kwa Preamble after reading this document unaweza kuweka maoni yako na ibadillishwe ama iongezwe. Yes okay, hata Programme Officer amenionyesha. Preamble, the Preamble should be simple and clear in language. Hii ilisemwa hapa Tigania West, sijui nani alisema hapa. Tulikuwa na many contributors, unajua report yenu, hapa Kianjai, Tigania West, ni report kubwa sana. One of the biggest, yaani ni namna hii. Niliona ya Tigania East ni kidogo, lakini ya hapa I think we had many contributors, na mlicover karibu nkila kitu. Mlisema the Preamble should be simple and clear in language. Ni mambo rahisi tu hakuna yale magumu ya kisheria. Na

ukiona ya Kiswahili, kwa sababu mtaiona kwa Kiswahili, that one itakuwa very clear. Na tena watu wa Kianjai hapa katika Tigania West walisema, The Preamble should state that Kenya is a God fearing country, and this is why we say God bless Kenya. That means, God bless everything, the preamble and Kenya, everybody. So we are God-fearing.

Then the Preamble should express the sovereignty of all Kenyans. This is inside here in the contents. Mambo yenu yote yako hapa na yamekuwa captured along with other constituencies. Sasa hicho ndicho kitu cha maana sana mtaona kwa hii.

Ningetaka kwenda kwa highlight ingine, ingine nitakuwa ninasoma kuchukua mfano, na ingine somebody else can read, na if you want to ask I can answer some of the questions and maybe explain. I would like to go to the point on language, that is section nine, okey now that is page 4 chapter two, under languages is article 9, hiyo ni mambo ya lugha. The official languages of Kenya are Kiswahili and English and all official documents shall be available in both languages. Na hayo tulisikia hata kutoka hapa, kila pahali. Watu wa Kenya wanasema lazima Kiswahili kiwe official language, na sasa tumeweka kwa Constitution Draft. Kiswahili and English shall be official languages of Kenya, and all documents shall be in Kiswahili and English. Mimi nimewaambia hii Draft yenyewe tunatengeneza na tuna-translate version ya Kiswahili, na Katiba kama wakati itakuwa ready iwe document kama hii, kitabu cha sheira, itakuwa na Kiswahili, na itakuwa na Kiingereza. Kwa hivyo wananchi wa Kenya waweze kusoma. Tukienda hata court, tutakuwa na form imeandikwa kwa Kiswahili na English. Ukitaka kufanya Kiswahili, all official documents kwa sababu lugha ikiwa official, tuseme kwamba itatumika kwa mambo rasmi ya serikali, mambo ya utawala na kila kitu. Tena ukiendelea hapo utaona imesema “The national language of Kenya is Kiswahili, na hapo lazima mjue kuna tofauti ya National language na official language. Official language ninawaambia ni kama documents zote, mambo yote ya utawala ndiyo yatakuwa na Kiswahili na English. Lakini mbeleni ilikuwa namna hiyo? This Constitution has never been translated in Kiswahili, na haingekubaliwa namna hiyo. Lakini hii itatokea sasa itakuwa kwa Kiswahili na itakuwa kwa Kiingereza, na vitabu vya sheria ambavyo ni vigumu vitakuwa kwa Kiswahili na vitakuwa hata kwa English. Yaani lugha zetu official ni mbili. Lakini tunaendelea hapa kusema Kiswahili kitakuwa national language, but it has been always like that. Kwa hivyo itaendelea kuwa national language.

National language ni kama kusema ni lugha ya taifa, kila mtu anaiongea. Hata ukiwa hujaenda shule unaongea tu Kiswahili. Ni lugha ya communication katika Kenya, ya watu wa kenya, Kiswahili. Na tumeona imekuwa promoted na inasemekana sasa itaingia hata kwa mambo ya utawala, ya kila kitu.

Mzee: (Inaudible)

Com. Ratanya: Sawasawa. Okay you will make your comments later, mzee anasema this draft does not discriminate our language. Kwa sababu imepatia Kiswahili huo uwezo wa kuwa official, na hiyo ni mzuri. Twende number three.

The state shall respect and protect the diversity and languages of the people of Kenya and shall promote development and use

of Kiswahili, indigenous languages, sign language and braille. Hii yote kutoka English, na Kiswahili ambacho ni official, tutaendelea ku-develop ama kukuza sana kufanya ziendelee vizuri, zifundishwe na kuwekwa hata lugha zetu, za Kimeru Kikuyu, Kiluhya, Kiluo. Hapo zamani kidogo tulikuwa tunajifunza hata Kimeru kwa ile inaitwa vernaculars, lakini ikamalizika kidogo kidogo hivi. Lakini sasa government yenyewe itakuwa sasa committed to develop the indigenous languages. Kama Kimeru itafunzwa hata zaidi, na lugha zingine zote. Lugha ya mikono hii mtu akiwa hajui kuongea sign language, hata hiyo itakuwa promoted na itatengenezwa. Braille, yale maandishi ya watu ambayo hawaoni. I think we have some copies here, Bwana Anampiu. If there is anybody who would like to have a copy of the brail we can give. Kuna mtu ambaye haoni, anataka Braille, kuna copy. Kwa hivyo hata hiyo baadaye serikali kulingana na Katiba vile inasema itaangalia lugha zote ziangaliwe na zifundishwe, na watu wajue. Ikiwa hauna mila wewe ni kama mtumwa, inasemekana namna hiyo. Na lugha ni kitu kimoja kuonyesha wewe ni nani--identity. Kwa hivyo hata lugha zetu zitakuzwa.

Lakini lugha zetu hazitakuwa official hata ingawa the Constitution itakuwa translated hata in Kimeru, mtasoma hata in Kimeru. Lakini haitakuwa official version. Official version ni nini? Ni Kiswahili na English. Lakini itakuwa translated in Kimeru, Kikuyu, I think we have started working on that. Inaendelea hapo headquarters. Wakati itamalizika, na tutakuwa na Katiba, tunaweza hata kusoma kwa lugha zingine. Na hii Katiba new haitakuwa inafichwa fichwa. Hii kuipata, sijui ni wangapi wako na copy kama hii? Mnajua pahali iko? Unless you go to government press, it is rather restricted. Ama uende kwa ofisi ya serikali. Lakini hii mpya itafanyiwa njia ya kila mtu ukitaka kununua ununue. Si mambo ya kufichwa ama kukataliwa kuwa nayo. Ukitaka kuisoma hata kwa Kimeru, kutakuwa na copies kama hizo. Ukitaka official copies za Kiswahili, utapata kununua, na hata za Kiingereza.

Tuende kwa highlight ya point ingine, kwa page 3 section 213.

TAPE 2:

Devolution of powers. We are looking for 213, two hundred and thirteen, article 213, devolution of power. Page 26, correct. Kuna hapo chapter 10, kuna devolution of powers. Hii ndiyo hata watu wa Tigania West walisema mkono moja usiwe na kila kitu. Yaani kila sheria ama power yote isiwe kwa mtu mmoja. Hii Katiba mpya imetengeneza power inaenda kwa watu wengi, inakuwa decentralized, inaenda, inasambazwa kutoka Central Government mpaka inaenda kwa watu. Na ningetaka volunteer atusomee especially if we start from the Organization of the Devolution Principles of devolved government, section 214. Nani anaweza kuwa volunteer asome hapa? Ninaona Mugambi pale, pengine kuna mwingine atasoma na yule. Okay, hebu anza Mugambi. Soma hapo 214.

